

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

*Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA*  
**Simu Na: +255 26 2321607**  
**Nukushi: +255 26 2322116**  
**Barua pepe: [ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)**



*Mji wa Serikali – Mtumba,  
Mtaa wa TAMISEMI,  
S.L.P. 1923,  
41185 DODOMA.*

**TAARIFA KWA UMMA**

**SIKU 4 ZAONGEZWA KUOMBA AJIRA ZA TAMISEMI**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa **Mhe. Innocent Bashungwa** ameongeza siku 4 kwa waombaji wa Ajira Kada za Elimu na Afya hivyo kwa sasa mwisho wa kuomba ajira hizo ni tarehe 08 Mei,2022 saa 5:59 usiku na sio tarehe 04 Mei,2022 kama ilivyotangazwa hapo awali.

Mhe. Bashungwa amesema ameongeza siku hizo ili wale wote walioshindwa kukamilisha maombi yao tangu Ajira hizo zilipotangazwa hapo tarehe 20 Mei,2022 kwa sababu zozote zile kutumia muda huu wa nyongeza kukamilisha maombi yao kupitia kiunganishi cha **[ajira.tamisemi.go.tz](http://ajira.tamisemi.go.tz)**

Akizungumzia idadi ya waombaji wa ajira hizo amesema mpaka kufikia tarehe 03.05.2022 saa 5:59 usiku waombaji waliokamilisha maombi yao kupitia mfumo kwa Kada ya Afya ni 39,053 na Kada ya Elimu ni 119,133 hivyo jumla ya waombaji wote ni 158,186.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipata Kibali cha Ajira cha watumishi 9,800 kwa Kada ya Ualimu na **7,612** kwa Kada ya Afya na tangazo la Ajira hizo lilitolewa tarehe 20.04.2022.

Waombaji walitakiwa kutuma maombi kuanzia tarehe 20 Aprili – 04 Mei,2022 hivyo kwa sasa mwisho wa kutuma maombi hayo ni tarehe 08 Mei,2022 saa 5:59 usiku.

Ajira hizi ni bure na hakuna gharama yeyote na endapo utapata changamoto yeyote wakati wa kuomba ajira hizi tafadhali wasiliana na Kituo cha Huduma kwa mteja kupitia **Namba 0735-160210 au 0262-160210 au tuma barua pepe kupitia [huduma@tamisemi.go.tz](mailto:huduma@tamisemi.go.tz)**

Nteghenjwa Hosseah  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Ofisi ya Rais –TAMISEMI  
03.05.2022